**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika; Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kutekeleza majukumu yetu kama tulivyojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika; Kwa mujibu wa Kanuni ya 109 (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambayo inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza katika Mkutano wa mwezi wa Febuari au wakati mwengine ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua.

Mheshimiwa Spika; Kamati ya Bajeti ilitekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Jadweli la Kwanza chini ya Kanuni ya 107(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilikutana na Wizara mbali mbali, Taasisi, Mamlaka, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali. Katika utekelezaji wa majukumu hayo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa Serikali na taasisi hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti imeundwa na Wajumbe saba (7), Makatibu Kamati watatu (3) na Msaidizi Mmoja (1) wa Mheshimiwa Mjumbe kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir (Mrembo) | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anna Athanas Paul | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 9. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 10. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 11. | Ndg. Yustina Edward Joseph | Msaidizi wa Mjumbe |

## MAUDHUI

**Mheshimiwa Spika;** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bajeti ilijielekeza zaidi katika kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji mapato na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Zanzibar.

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI

### Mfumko wa Bei

Mheshimiwa Spika; Katika mwaka 2021, Mfumko wa Bei ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 kwa mwaka 2020. Mfumko wa Bei umeendelea kupungua na kubaki katika kiwango cha tarakimu moja. Hali hii inasaidia kuendelea kuwepo kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Spika; Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii sambamba na kuishauri kuendelea na udhibiti wa bei ya mafuta kulingana na bei ya soko la dunia, ihakikishe upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko yetu pamoja na kuongeza juhudi za kuuza bidhaa zetu nje ya nchi ili kuwe na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ili kuendelea kuudhibiti mfumko wa bei.

### Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania

Mheshimiwa Spika; Thamani ya Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu ikilinganishwa na sarafu nyengine duniani na nchi washirika wa biashara. Katika kipindi cha Disemba 2021, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2309.24, ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,309.99 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika; Utulivu wa Sarafu ya Tanzania unatokana na kuwepo kwa mfumko wa bei wa chini ambao unaendana na vigezo na matakwa ya jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwepo kwa sera bora za fedha na uchumi Tanzania.

### Idadi ya Watalii

Mheshimiwa Spika; Kumekuwa na ongezeko la watalii mwaka 2021 kwa kufikia watalii 394,185 kutoka watalii 260,644 waliongia katika mwaka 2020. Kuongezeka kwa idadi ya watalii katika mwaka 2021 imechangiwa zaidi na kuwepo kwa chanjo ya UVIKO 19, ambayo imepelekea baadhi ya nchi kuondosha

vikwazo vya kusafiri katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika; Ni wazi kuwa, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta zinazokuwa kwa kasi sana Zanzibar na ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, bado kuna changamoto za msingi ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi kwa haraka ili sekta hii kuwa na mafanikio. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali, kutengeneza mfumo utakaowezesha kujua mapato yote yanayotokana na sekta ya utalii tokea mgeni anapowasili mpaka atakapoondoka.

## Maoni na Ushauri wa Jumla wa Kamati

Mheshimiwa Spika; Kamati inasisitiza umuhimu wa kuzingatia ukuaji wa uchumi unagusa sekta zinazoajiri wananchi wengi ili kupunguza umaskini kwani licha ya kwamba Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi kuonesha kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar, bado kuna changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa ukuaji huu unaenda sambamba na upunguzaji wa umaskini.

Mheshimiwa Spika; Takwimu za mwenendo wa hali ya uchumi zinaonesha mafanikio katika sekta mbali mbali za kiuchumi lakini bado kumekuwepo na malalamiko ya hali ngumu ya kimaisha kwa wananchi wengi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha takwimu zinazokusanywa na kufanyiwa uchambuzi zina uhalisia na zinaakisi hali halisi.

# TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021 NA NUSU MWAKA (JULAI – DISEMBA 2021/2022)

## Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika; Takwimu zinaonesha kwamba, hadi kufikia Juni, 2021, mapato ya Serikali yalifikia TZS 940.2 bilioni sawa na asilimia 59.5 ya lengo la kukusanya TZS 1,579.2 bilioni. Matumizi ya kazi za kawaida yalikuwa TZS 740.1

bilioni ambayo sawa na asilimia 77.6 na matumizi ya kazi za maendeleo yalikuwa TZS 213.7 bilioni sawa na asilimia 22.4 ya kiasi kilichopangwa kutumika.

Mheshimiwa Spika; Kiwango hiki cha makusanyo ya mapato si cha kuridhisha ukilinganisha na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni vyema Serikali ikafanya jitihada ya kutafuta maeneo mengine ya vyanzo vya mapato (potential areas) sambamba na kukusanya kwa ufanisi ili iweze kugharamia bajeti yake iliyopangwa na hivyo kukidhi mahitaji halisi ya wananchi.

## Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa Nusu Mwaka wa 2021/2022 (Julai – Disemba 2021/2022)

Mheshimiwa Spika; Kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022 (Julai – Disemba 2021), Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 466.5 bilioni sawa na asilimia 69.3 ya makadirio ya TZS 672.8 bilioni kwa kipindi hicho, na asilimia 25.3 ya makadirio ya TZS 1,845.6 bilioni kwa mwaka mzima wa 2021/2022. Matumizi halisi ni TZS 367.9 bilioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 79, na kwa upande wa matumizi ya kazi za maendeleo zimetumika TZS 97.6 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 21 ya jumla kilichokusanywa.

Mheshimiwa Spika; Hali hii ya ukusanyaji wa mapato hairidhishi, ni vyema Serikali ikapanga makadirio yenye uhalisia kulingana na uwezo wetu wa ukusanyaji mapato badala ya kuweka malengo makubwa ambayo hatuwezi kuyafikia.

## Deni la Taifa

Mheshimiwa Spika; Hadi kufikia Disemba 2021, Deni la Taifa limefikia TZS 1,127.5 bilioni ikilinganishwa na TZS 896.6 bilioni Disemba 2020. Hii inamaanisha kwamba, kwa kipindi cha mwaka mmoja Deni la Taifa limeongezeka kwa TZS

230.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 25.6.

**Mheshimiwa Spika;** Pamoja na kuwa deni hili ni himilivu kwa vigezo vyote bado limekuwa ni mzigo mkubwa kwa nchi yetu kwani limekuwa likiongezeka kila mwaka. Kamati inaishauri Serikali, kukopa mikopo yenye masharti nafuu sambamba na kuzielekeza fedha za mikopo katika miradi itakayochochea ukuaji wa uchumi.

### Uimarishaji wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfumo wa Kukusanya Mapato ya Serikali kwa njia ya kielektroniki (ZanMalipo) na kuanza rasmi matumizi ya Mashine za Kielektroniki za Utoaji wa Risiti (VFD's). Kamati inasisitiza kwamba, changamoto mbali mbali ambazo zimejitokeza katika kutumia mifumo hiyo zitatuliwe kwa haraka ili mifumo hiyo iwe endelevu na iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

## UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

**Mheshimiwa Spika;** Kwa madhumuni ya kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji bora wa bajeti za Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ili kufikia lengo la ukusanyaji mapato na matumizi kwa ufanisi na pia kuweza kutoa gawio kwa Serikali. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti za Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kama yanavyoonekana katika Ripoti ya Kamati ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imebaini kwamba, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma katika kutekeleza bajeti na majukumu yake zinakabiliwa na changamoto

mbali mbali kama vile:

i. Taasisi na Mashirika ya Umma kukabiliwa na madeni makubwa.
ii. Uhaba wa vitendea kazi.
iii. Uhaba wa wafanyakazi wenye weledi.
iv. Uhaba wa fedha kutoka Serikalini
v. Kuwepo kwa ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi.
vi. Kukosekana kwa mifumo ya TEHAMA itakayosaidia katika uendeshaji wa shughuli.
vii. Kuchelewa kwa taratibu za zabuni.
viii. Kuchelewa kwa mafunzo kwa watendaji.
ix. Kusuasua katika utekelezaji wa miradi.
x. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika; Ili malengo ya Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma yaweze kufikiwa, Kamati ya Bajeti inashauri mambo yafuatayo:

i. Serikali inapaswa kuweka mipango na mikakati madhubuti inayotekelezeka ili itakayosaidia Mashirika kujiendesha kibiashara na kuweza kutoa gawio kwa Serikali.
ii. Serikali iweke mpango maalumu wa kuhakikisha taasisi na mashirika yanapatiwa majengo kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
iii. Serikali izipatie taasisi na mashirika rasilimali fedha za kutosha, vitendea kazi na rasilimali watu ili mafanikio na tija ya kuanzishwa kwao yaweze kufikiwa.
iv. Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma yapange na kutekeleza mipango ya mafunzo kwa watendaji wao.

## UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti katika kutambua na kuthamini mchango wa Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli zake na uchangiaji wake katika shughuli za maendeleo ilipokea taarifa za mapato na matumizi ya Baraza la Mji Chake Chake, Baraza la Mji Mkoani, Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Micheweni kwa upande wa Pemba na Baraza la Mji Kaskazini "A" na Baraza la Mji Kaskazini "B" kwa upande wa Unguja, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika;** Mabaraza ya Miji na Halmashauri ya Unguja na Pemba zinakabiliwa na changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa bajeti na majukumu yake, hali inayoathiri ufanisi katika utendaji kazi. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

i. Kutopatiwa ruzuku ya matumizi mengineyo kwa baadhi ya Mabaraza na Halmashauri.

ii. Matumizi kwa miradi ya maendeleo hayaridhishi, matumizi mengi yanakwenda kwenye shughuli za uendeshaji wa ofisi.

iii. Vyanzo vya mapato vya mabaraza kusimamiwa na taasisi nyengine kama vile mapato ya vibali vya ujenzi, maliasili na vituo vya mafuta.

iv. Kuchelewa kwa marejesho ya mapato kutoka Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi Zanzibar (DCU), Idara ya Maliasili, ZURA na Bodi ya Vileo.

v. Upungufu wa watumishi wenye weledi katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato

vi. Mfumo wa kukusanyia mapato wa ZanMalipo kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa POS za kutosha na hitilafu za kimtandao.

vii. Kukosekana kwa vyanzo vya kudumu vya mapato vinavyotokana na miradi ya kiuchumi iliyoanzishwa na Mabaraza au Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika;** kwa lengo la kupata utatuzi wa changamoto zinazoyakabili Mabaraza ya Miji na Halmashauri. Kamati ya Bajeti inashauri mambo yafuatayo:

i. Kamati inayasisitiza Mabaraza ya Miji na Halmashauri kuendelea kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo lililokusudiwa.
ii. Kamati inayashauri Mabaraza ya Miji na Halmashauri kusimamia matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti upotevu wa mapato hayo.
iii. Kamati inayashauri Mabaraza ya Miji na Halmashauri kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa jamii ili mapato yanayokusanywa kwa wananchi yaweze kuwaondolea kero mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinazowakwaza katika maisha ya kila siku.
iv. Kamati inaishauri Serikali kuajiri vijana wenye sifa kwa lengo la kuzisaidia Mamlaka hizi katika uendeshaji wa shughuli zake ili zifikie malengo waliojiwekea.
v. Kamati inaishauri Serikali kuwayapatia ruzuku stahiki Mabaraza ya Miji.
vi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuishajihisha jamii katika kudai risiti pindi wanapotozwa tozo na ada mbali mbali.
vii. Kamati inaishauri Serikali kusimamia marejesho ya mapato ya Mabaraza yaliyokusanywa na DCU, ZURA na Idara ya Maliasili.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

### Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala ya kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali

ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi kuwekeza. Ushiriki wa Sekta binafsi katika miradi ya maendeleo unapunguza gharama ya Serikali katika kugharamia miradi hiyo na pia inachochea kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika; Ili kuwezesha kuimarika kwa sekta binafsi, Serikali ihakikishe inasaidia kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo. Miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta binafsi ni:-

i. Wingi wa mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi.
ii. Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi.
iii. Wingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja.
iv. Kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika; Ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kuwaondeshea usumbufu sekta binafsi wa kuwepo utitiri wa mamlaka za udhibiti na wingi wa tozo na kodi, Kamati inashauri kuwepo mamlaka moja au chache za udhibiti wa biashara na kuwepo kodi moja ambayo baadae kila mamlaka husika ipate mgao wake. Aidha, Kamati inashauri kuimarishwa maeneo ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

## MIRADI YA MAENDELEO ILIYOFANYIWA KAZI NA KAMATI YA BAJETI

Mheshimiwa Spika; Kamati ya Bajeti ilipokea taarifa za miradi ya maendeleo mbali mbali ambazo ilizichambua kwa kina na kuikagua miradi hiyo na kubaini changamoto zinazojitokeza katika kutekeleza miradi hiyo na hatimae kuweza kutoa maoni na ushauri kwa taasisi zinazotekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika; miongoni mwa changamoto zinazoathiri utekelezaji wa miradi kwa taasisi zetu na ambazo zinastahiki kupatiwa ufumbuzi ili mafanikio na tija iliyokusudiwa iweze kufikiwa ni kama hizi zifuatazo:

i. Mripuko wa ugonjwa wa UVIKO 19 uliathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa

mradi kwani ilipelekea kusitishwa kwa mafunzo pamoja na kuondoka na kuchelewa kurudi mshauri mwelekezi.

ii. Kuchelewa kwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kutokana na hatua za kibenki zinazohitajika kufanywa kabla ya fedha hizo kutoka.
iii. Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo, kuzipatia taasisi husika fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Kutokupatikana kwa fedha za mradi kunazorotesha utekelezaji wa miradi na hatimae kushindwa kukamilika na kuwanufaisha wananchi kwa wakati.
iv. Kutokukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi kwa baadhi ya maeneo.
v. Kutokuwajibika ipasavyo kwa mshauri elekezi wa mradi katika kusimamia kazi hali inayochangia kutogundua kasoro zinazojitokeza kwa wakati katika utekelezaji wa mradi.
vi. Kuchelewa utekelezaji wa mradi kulikotokana na kukwama kwa taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Spika; Ili Taasisi zinazotekeleza Miradi ya Maendeleo ziweze kutekeleza = miradi hiyo kwa ufanisi hakuna budi kutafuta ufumbuzi wa kuzitatua changamoto zinazozikabili. Katika kufikia utatuzi wa changamoto hizo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

i. Panapokuwa na changamoto zozote kama vile mripuko wa UVIKO 19, kuwepo na njia mbadala za kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.
ii. Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo, kuzipatia taasisi husika fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Kutokupatikana kwa fedha za mradi kunazorotesha utekelezaji wa miradi na hatimae kushindwa kukamilika na kuwanufaisha wananchi kwa wakati.
iii. Kamati inaishauri taasisi zinazotekeleza miradi kuwa na timu za ufundi

(Technical Team) zitakazosaidia usimamizi na kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa za mradi.

## MAONI NA USHAURI WA JUMLA WA KAMATI KWA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti katika kufuatilia na kusimamia majukumu yake katika Wizara na Taasisi mbali mbali imebaini mafanikio na changamoto zilizopo katika taasisi hizo. Kamati kupitia chombo hichi kitukufu kinapenda kutoa shukurani zake za dhati kwa taasisi zilizofanya majukumu yao ipasavyo na pia inachukua fursa hii ya kutoa maoni yake ya jumla kwa lengo la kuimarisha utendaji wa taasisi zetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida Serikali katika kutekeleza majukumu yake inahusisha upangaji wa maeneo ya vipaumbele kwa lengo la kuharakisha ukuaji wa maendeleo na uchumi wa nchi pamoja na kuhakikisha kuwa huduma bora na ustawi wa jamii unafikiwa kwa wote. Kamati inaunga mkono utaratibu huu nzuri uliopo na inaishauri Serikali kuzingatia upangaji wa vipaumbele vichache vitakavyoweza kutekelezwa kulingana na uwezo wa mapato yetu ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea taasisi mbali mbali za Serikali pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo imebaini upatikanaji mdogo wa fedha katika miradi hiyo hali inayorudisha nyuma utekelezaji wake. Katika kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kutiliwa mkazo utekelezaji wa Miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (**Public Private Partinaship - PPP**) ili kukabiliana na ufinyu wa bajeti na kuiwezesha Serikali kufikia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya kimaendeleo na kutoa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kufanikiwa kwa sekta ya miundombinu nchini kunategemea sana upatikanaji wa fedha zinazostahiki katika kuiendeleza sekta hiyo. Kamati imebaini upatikanaji mdogo wa fedha za bajeti katika sekta hii kunachangia

kutotekelezwa kwa ujenzi wa miundombinu na pia kutokuwa na uimara wa miundombinu hiyo ikiwemo ubovu wa barabara katika baadhi ya maeneo yetu na kushindwa kuendelezwa kwa miundombinu mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kupambana na hali hii, Kamati inashauri Serikali kuingiza fedha za bajeti kwa wakati ili ziweze kutumika katika kufanikisha shughuli zilizokusudiwa sambamba na kuwataka watendaji kufuata taratibu zinazotakiwa katika kutumia fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na tathmini na ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kutekeleza miradi ya maendeleo nchini inayohusisha sekta mbali mbali ikiwemo elimu, afya na kilimo. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaitaka Serikali kutunga Sheria mahsusi inayohusiana na Tathmini na Usimamizi wa Miradi kwani kutungwa kwa Sheria hiyo kutaweza kusaidia katika usimamizi nzuri wa miradi inayotekelezwa. Aidha, Kamati inazitaka taasisi mbali mbali za Serikali kuhakikisha utekelezaji wa miradi yao inalenga katika kutoa huduma inayokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa mapitio ya Sera na Mpango Mkakarti wa Uchumi wa Buluu kunazorotesha katika kufikia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uchumi wa Buluu ikiwemo kusimamia, kuratibu na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa buluu nchini. Kamati inaitaka Serikali kusimamia ukamilishwaji wake kwa kuhakikisha fedha za utekelezaji wa shughuli hiyo zinapatikana kwa wakati na adhma ya Serikali yetu katika sekta ya uchumi wa buluu iweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea Mabaraza na Halimashauri kwa Unguja na Pemba imebaini changamoto ya upatikanaji fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa vile miradi mingi inashindwa kukamilishwa kutokana na ukosefu wa fedha, hivyo waheshimiwa wajumbe waliopo katika majimbo kusaidia kwa baadhi ya Miradi. Kwa msingi huo, Kamati inaomba kuongezwa kwa

fedha za Mfuko wa Jimbo ili ziweze kusaidia katika kukamilisha miradi ya aina hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaomba kuanzishwa kwa Kurugenzi ya Bajeti katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi ili iweze kusaidia katika kuleta ufanisi zaidi wa kazi za Kamati katika maeneo mbali mbali ikiwemo ya kibajeti na Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo kiasi ambacho ufanisi unakosekana katika utekelezaji wake na gharama inaongezeka. Kamati inashauri, ni bora tupange miradi michache lakini tutakayoweza kuitekeleza ili kumaliza kwa wakati na kuanza kutoa tija sambamba na kuepuka kuongezeka kwa gharama kunakosababishwa na kuchelewa kumalizika kwa mradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya matumizi ya Serikali yanaonesha kwamba, fedha nyingi zinatumika katika matumizi ya kawaida ukilinganisha na fedha zinazotumika katika kazi maendeleo, hali hii inapelekea kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa ikizingatiwa kwamba upatikanaji wa fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo si wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuanzisha chombo maalum ambacho kitahusika na kutambua vyanzo vyote vya mapato na kuweka makisio ya mapato kwa kila mwaka kwa taasisi zote za Serikali na Mashirika ya Umma. Hii ni kutokana na kila taasisi au Shirika kujipangia makisio ya mapato yake wenyewe. Hali hii husababishwa taasisi au Shirika kuweka makisio madogo ya kukusanya mapato ili kuonekana zimevuka lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Mabaraza na Halmashauri zinatofautiana vyanzo vya ukusanyaji mapato licha ya kwamba upo uwezekano wa kutekelezeka vyanzo vinavyolingana katika Mabaraza na Halmashauri zote. Hali hii inatokana na kukosekana kwa mazingatio mazuri kwa baadhi ya vyanzo vya mapato au kutoripotiwa kwa taarifa za mapato kutoka katika vyanzo hivyo. Kamati inaishauri Serikali, kukaa na Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Manispaa zote za Zanzibar na kuorodhesha vyanzo vyote vya mapato vinavyoweza

kukusanywa na Baraza, Halmashauri au Manispaa husika pamoja na kuweka makisio ya makusanyo kwa kila chanzo. Taarifa ya vyanzo vyote vya mapato na makadirio yake kwa kila Baraza, Halmashauri na Manispaa yawekwe katika Hotuba ya Bajeti kila mwaka.

## HITIMISHO

Mheshimiwa Spika; Naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kwa kuliendesha Baraza hili la Wawakilishi kwa weledi mkubwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jamal Kassim Ali Waziri Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao waliyoipatia Kamati katika vipindi vyote vya mzunguko wa kazi za Kamati. Nawashukuru pia Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi nyengine zilizofanya kazi na Kamati kwa mashirikiano yao mazuri na hatimae kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika; Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inaisimamia vyema Serikali.

Mheshimiwa Spika; Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru watendaji wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza Bi. Raya Issa Msellem, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Kamati ya Bajeti naomba kuwasilisha. Asanteni kwa kunisikiliza.

……………………………….
Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.